HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA (JAJI MKUU) KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA KITABU CHA WASIFU NA MAISHA YA MAREHEMU JAJI WA RUFANI ROBERT HABESH KISANGA

JULIUS NYERERE INTERNATIONAL CONVENTION CENTRE (UKUMBI WA RUAHA)

TAREHE 23 JANUARI 2024

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani mliopo,

Mhe. Barnabas Samatta Jaji Mkuu Mstaafu,

Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu,

Mhe. Khamis Ramadhan Abdallah, Jaji Mkuu wa Zanzibar,

Wahe. Majaji wa Rufani Wastaafu,

Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi,

Wahe. Majaji Viongozi wastaafu mliopo,

Mama Maria Ezra Kisanga, Mjane wa Jaji Robert Kisanga,

Familia ya Marehemu Mhe. Jaji Kisanga,

Wahe. Majaji Wafawidhi wote mliopo,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu mliopo,

Wahe. Majaji Wastaafu mliopo,

Mhe. Sylvester Kainda, Msajili wa Mahakama ya Rufani na Kaimu Msajili Mkuu,

Wahe. Makatibu Wakuu wote mliopo,

Mhe. Projestus Kahyoza, Kaimu Msajili Mahakama Kuu,

Wahe. Naibu Wasajili wote,

Watendaji wote wa Mahakama Kuu,

Wageni waalikwa wote mliopo,

MAHAKAMA YA TANZANIA!!—UADILIFU, WELEDI, UWAJIBIKAJI

- Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema kuweza kukusanyika asubuhi hii kuzindua kitabu, kuhusu **Ndoto iliyozaa Matunda: Maisha ya Jaji Robert Habesh Kisanga**.

- Ni siku ya furaha siku ya leo, hafla hii ya kusherehekea Maisha ya **ROBERT**, **MTOTO WA KIUME WA MTOURE (LERINYO)** kutoka **UKOO WA KISANGA**, aliyepewa **JINA LA UTANI (NICKNAME) "HABESH.**"
- Ametukutanisha hapa, wengine hatujakutana kwa miaka mingi.
- Sina uhakika kama kuna yeyote kati yetu hapa, anaweza kumkumbuka Jaji Robert Kisanga na kumzungumzia kama

Jaji MWENZAKO *(contemporary)*. Wote tunamzungumzia Jaji Kisanga kama vile MWALIMU WETU WA UTAWALA WA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU.

- Kwa mfano, wakati wa Mahojiano Maalum baina JAJI Joseph Sinde WARIOBA na Dkt. Faustine Kihwelo wakati wa matayarisho ya Sherehe za Miaka 100 tangu kuanzishwa kwa Mahakama Kuu, Jaji Warioba alikumbusha kuwa ALIFUNDISHWA KAZI katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wanasheria aliowakuta huko, wakiwemo, ROBERT HABESH KISANGA na YONA MWAKASENDO ambao walikuwa BARRISTER-AT-LAW waliosomea Sheria huko Uingereza. Jaji Warioba **(LLB Class 1963-1966)**[1] alimueleza Dkt. Kihwelo yafuatayo: *"Mwakasendo alipata kuwa Deputy Attorney General. Lakini Kisanga alikuwa Senior State Attorney. Na kweli hawa, wakati huo ilikuwa ni nguzo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa hiyo walikuwa senior. Lakini ilipoonekana kuna mahitaji ya kupata Majaji wenye qualification wengi walichukuliwa kutoka Idara nyingine za Serikali, na zaidi walichukuliwa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu."*

[1] Kanywanyi, JL., Kolimba, H., Lubuva, D., Samatta, B.A.,

- Ukisoma *High Court Digests (HCD)* za mwaka 1970 na 1971, unaweza kuwatambua nani walikuwa contemporaries wa Jaji Kisanga ambao waliweza kuitana kwa majina ya kwanza na hata kutaniana kwa majina ya utani—**Kisanga, Ag. J. (Kaimu Jaji)**; **Kwikima, Ag. J.**; **Mnzavas, Ag. J.**; **El-Kindy, Ag. J.**; **Jonathan, Ag. J.**; **Mwakasendo, Ag. J.**; na **Patel, Ag. J**.

- Napenda kutambua mchango mkubwa familia ya Jaji wa Rufani Robert Habesh Kisanga wakiongozwa na Mama Ezra Kisanga, ambao kwa takriban miaka mitano, wameshirikiana na Chuo Cha Uongozi wa Mahakama kukusanya na kuiweka katika maandishi historia ya Maisha na Wakati wa Jaji wa Marehemu Robert Habesh Kisanga.

- Familia ya Jaji Kisanga, kupitia *Architect* (Msanifu) Mtoure Kisanga, ndio waliibua wazo la kitabu cha Maisha ya Jaji Kisanga. Sisi Mahakama, tukaona kuwa tuna mengi ya kujifunza kutoka katika Maisha na Wakati wa Jaji Robert Kisanga: ***what a great way to begin chronicling our***

history through biographies and autobiographies of the judicial actors who served the Judiciary, Tanzania, and Africa with colossal distinction?

- *Architect* (Msanifu) Mtoure Kisanga alikuwa akifuatilia sana hatua mbali mbali utayarishwaji wa Kitabu, na mara zote huomba kuwa nimruhusu awe ananikumbusha.

- Aidha, Napenda kuwashukuru wote ambao wamefanya kazi kubwa, kazi ambayo matunda yake ni Kitabu. Tusingeweza kukutana hapa kama sio kazi kubwa na juhudi zilizofanywa Jaji wa Rufani ambaye pia ni Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, DKT. FAUSTINE KIHWELO. Tumpongeze sana Mkuu wa Chuo, amesogeza wigo wa shughuli za Chuo Cha Uongozi Mahakama na Chuo kimaeahidi kuendeleza utamaduni wa kuandika historia ya Tanzania na historia ya Mahakama ya Tanzania kupitia Historia ya Maisha ya Majaji. Dkt. Faustine Kihwelo, nakushukuru sana kwa neno lako la ukaribisho katika hafla hii.

- Ningependa kuwashukuru pia, Jaji Frank Mirindo na Dkt. Clement J. Mashamba, Mhadhiri Shule ya Sheria kwa

Vitendo. DKT. KIHWELO, JAJI MIRINDO na DKT. MASHAMBA ndio waliotayarisha kitabu nitakachozindua muda mfupi ujao.

- Kwa namna ya kipekee, naomba kwa kipekee kumshukuru Mhe. DKT. FAUZ TWAIB (Jaji Mstaafu), kwa maelezo kuhusu Kitabu, ambayo yametupa hamasa, sio tu kukinunua, bali pia kukisoma. **NB—*THE ETIQUETTE OF BOOK LAUNCHES* by HAZEL EDWARDS—"If you agree to launch it: (1) Read ALL the book, preferably before you say 'ÝES, I will launch it.'**

- Baada ya kusikiliza maelezo ya Dkt. Fauz kuhusu Kitabu, wote tuliopo hapa tunaweza kusema kuwa KITABU KUHUSU MAISHA NA WAKATI WA JAJI ROBERT HABESH KISANGA kimesheheni mambo mengi ya kujifunza au hata kuyafuatilia na kuyaelewa.

- Kitabu hiki kinatukumbusha ukweli kuwa ni kwa kurejea historia ya sheria, ndio utaweza kuelewa sheria zilizopo sasa. Huwezi kuelewa historia ya Sheria kwa kuzitenganisha na

Maisha ya viongozi walioongoza na kusimamia hizo sheria na hizo taasisi. MAISHA NA WAKATI WA JAJI ROBERT HABESH KISANGA yamefungamana na historia za Taasisi nyingi ndani na nje ya Tanzania.

- Kupitia kurasa za kitabu hiki cha Maisha ya Jaji Robert Kisanga:
    - ***we see the life of a focused, determined person. Robert Habesh Kisanga was laser-focused on studying law and ultimately joining legal practice.***
    - ***Although he was doing better in sciences at Makerere University intermediate courses, he settled on arts courses because these were his road to his Damascus that is, practice in law.***
    - ***So focused on his legal profession, he declined an opening to join the Bank of Tanzania and preferred lower-paid work as a State Attorney.***

- ***When you look back on Justice Kisanga's decision to focus on law, it may not have been very welcome to his***

family financially. Still, that focus was very beneficial to Tanzania and Africa.

MAREHEMU JAJI ROBERT HABESH KISANGA ALIACHA ALAMA ISIYOFUTIKA ZAIDI YA KWENYE MCHANGA WA HAKI:

- Wanadamu wa Kale huko Ngorongoro, waliotembea kwenye tope na majivu ya volcano yaliyokuwa hayajakauka zimetupa viashiria vya namna walivyoishi. Wanadamu wa leo wanaacha historia ya kesho, kupitia maandishi.

    - Jaji Mkuu Mstaafu wa Ghana, Jaji Anin Yeboah, aliwahi kuwaasa Majaji wa Mzunguko *(Circuit Judges)* na Mahakimu aliokuwa akiwaapisha, kuwa wafanye kazi za utoaji haki kwa bidii na juhudi kubwa na wajitoe muhanga waache alama isiyofutika katika mchanga wa Haki:— *"You are required to leave an indelible mark in the judicial sands of time and you can only achieve this through exceptional effort and great sacrifice..."*

- Marehemu Jaji Robert Habesh Kisanga aliacha alama yenye wino usiofutika katika Katiba ya Tanzania hususan mchango wake katika **MABADILIKO YA KUMI NA TATU NA KUMI NA**

NNE KATIKA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WA MWAKA 2004.

- Akisoma Muswada wa Mabadiliko ya Kumi na Nne, WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA (Harith Mwapachu) alieleza wazi kuwa:
    - Msingi wa mapendekezo ya mabadiliko haya [ya 14] ni kuendelea kutekeleza maoni ya wananchi yaliyoratibiwa na **Kamati ya Jaji Robert Kisanga**, iliyokusanya maoni kuhusu hoja 19 kupitia Waraka wa Serikali namba 1 wa mwaka 1998 yaani *White Paper.*

    - Waziri Harith Mwapachu alifafanua kuwa, baada ya kupokea taarifa hiyo, Serikali ililieleza Bunge kwamba maoni ya wananchi yalikuwa ni muhimu na mazito na hivyo utekelezaji wake ungefanywa **KWA AWAMU**.

    - **AWAMU YA KWANZA** ilianzia na MABADILIKO YA KUMI NA TATU yaliyopitishwa na Bunge mwaka 2000 yalilenga katika kuimarisha demokrasia hasa mchakato wa uchaguzi.

- **AWAMU YA PILI** ya kutekeleza maoni ya wananchi yaliyokusanywa na Kamati ya Jaji Robert Habesh Kisanga yalipitia Mabadiliko ya Kumi na Nne ambayo yalikuwa na shabaha ya kuhakikisha kwamba Ibara za Katiba zinazohusu haki za binadamu na wajibu wa watu ulioainishwa katika sehemu hiyo zinaandikwa vizuri zaidi ili kulinda na kuhifadhi haki hizo kwa namna ambayo inasomeka vizuri zaidi na kuzingatia maoni ya wananchi kama yalivyoratibiwa na Kamati ya Jaji Robert Kisanga. Baadhi ya mapendekezo yaliyomo katika Muswada wa Mabadiliko ya Kumi na Nne kuboresha uandishi wa Ibara za Katiba zilizohusu Haki za Binadamu.

- **MOJA YA ALAMA KUBWA** zilizoletwa na Jaji Kisanga kupitia Mabadiliko ya Kumi na Tatu ya Katiba ni kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ***(The Commission of Human Rights and Good Governance)***, ambayo ilianzishwa chini ya Ibara ya 129.

- Na Jaji Kisanga aliacha alama nyingine mara baada Mhe. Rais Benjamin William Mkapa kumteua, Mwaka 2002 **KUANZISHA TAASISI MPYA KABISA TANZANIA,** kama Mwenyekiti wa kwanza wa **TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**.

IJA ENDELEZENI UTAMADUNI HUU

- Nimalize kwa kukiomba Chuo cha Uongozi wa Mahakama, kiendeleze huu utamaduni wa kuandika katika vitabu, alama za historia, zisizofutika ambazo Majaji na Watumishi wengine wa Mhimili wa Mahakama wameacha.

- Naomba nimalize kwa kupendekeza kwenu kitabu kuhusu Maisha, Wakati na Ndoto za Marehemu Jaji Robert Hasbesh Kisanga na kuwashukuru tena, kwa kuhudhuria. Ninaamini kuwa kila mmoja wenu atakinunua kitabu hiki.

- Utakaposoma kitabu hiki, fuatilia *footnotes*, na picha mbali mbali, utagundua bado kuna maeneo mengi ya maisha ya Jaji Robert Habesh Kisanga ambayo, bado yanasuibiri kusimuliwa na kufafanuliwa. Nyayo za Jaji Robert Habesh Kisanga zimetapakaa katika michanga ya aina nyingi

ambayo yalileta mabadiliko na maboresho katika maisha ya Tanzania na Watanzania. Kwa mfano, Ripoti ya Tume ya Jaji Kisanga kuhusu ajali ya Meli ya MV Bukoba, hapana shaka ilifuatiwa na mabadiliko mengi katika usalama wa vyombo vya usafiri majini.

- Naomba nimrudishie Mshereheshaji aendelee na programu hii.

Ahsanteni kwa kunisikiliza